



TANZANIA REVENUE AUTHORITY

TAAARIFA KWA UMMA

UHUISHWAJI WA MFUMO WA TANCIS

Dar es Salaam, 28 Januari, 2025

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwatangazia walipakodi wote kuwa Tarehe 20 Januari, 2025 mfumo wa Forodha (TANCIS) ulioboreshwa ulizinduliwa ambao utakuwa unatumika badala ya Mfumo uliokuwa ukitumika zamani, ili kurahisisha huduma za kiforodha na kupunguza gharama kwa waagizaji na wasafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi pamoja na wadau mbalimbali.

Tunawashukuru wadau wote na Umma kwa ujumla kwa ushirikiano mlioonesha katika kipindi chote cha maboresho ya Mfumo wa TANCIS. Mfumo huu unafanya kazi sasa ipasavyo, na tunatambua baadhi ya watumiaji kuwa bado wanapata changamoto kadhaa.

Kwa kutambua changamoto zilizojitokeza wakati wa mabadiliko ya mfumo huu na ili kuboresha mashirikiano na wadau wetu, **Mamlaka ya Mapato Tanzania itaondoa, kwa mujibu wa Sheria, gharama za utunzaji wa mizigo zitakazothibitishwa kutokana na changamoto za uhuishwaji wa mfumo huu. Pia, itashirikiana na wadau wa bandari kavu (ICDs) na viwanja vya ndege ili kuondoa gharama za utunzaji wa mizigo zitakazothibitishwa kutokana na mabadiliko haya.**

TRA inaendelea kuwahakikishia wadau na walipakodi kuwa wanaweza kuendelea kutumia mfumo wa TANCIS ulioboreshwa bila kuwa na wasiwasi wowote.

Kwa maelezo na msaada zaidi, tembelea kituo cha huduma kwa wateja kilichopo **Ghorofa ya 4, jengo jipya la bandari (TPA)** au wasiliana nasi bure kwa simu namba **0800750075, 0800780078 au 0800110016.**

"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"

Yusuph Juma Mwenda
Kamishna Mkuu